Jinsi Ninavyotaka Nikutwe Na Kristo

Na

Ellis P. Forsman

(How I Want To Be Found By Christ)

Jinsi Ninavyotaka Nikutwe Na Kristo

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Jinsi Ninavyotaka Nikutwe Na Kristo

Fil. 3:8-9

Biblia (Agano la Kale na Jipya) inafundisha kwamba Kristo anakuja.

- Mat. 25:31, "*Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake;*"
- 2 Thes. 2:1-3, "*Basi ndugu tunakusihini, kwa habari ya kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, na kukusanyika kwetu mbele zake, kwamba msifadhaishwe upesi hata kuiacha nia yenu, wala msisitushwe, kwa roho, wala kwa neno, wala kwa waraka unaodhaniwa kuwa ni wetu, kana kwamba siku ya Bwana imekwisha kuwapo. Mtu awaye yote asiwadanganye kwa njia yoyote; maana haiji, usipokuja kwanza ule ukengeufu, akafunuliwa yule mtu wa kuasi, mwana wa uharibifu.*"
- Mat. 24:35-39, "*Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe. Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana ila Baba peke yake. Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya gharika watu walivyokuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.*"

Hajasema KAMA akija, lakini amesema ATAKAPO kuja. Atakutaje kila mmoja wetu?

Jinsi ninavyotaka nikutwe na Yesu kama akirudi nikiw hai?

Nataka nikutwe ndani yake

Hivi ndivyo Paulo alivyotaka akutwe.

Fil. 3:8-9, "*Naam, zaidi ya hayo nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo; <u>tena nionekane katika yeye</u>, nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani.*"

Kwa nini ni muhimu kukutwa katika Kristo?

Ni matumaini ya mtu kwa ajili ya uzima wa milele.

Yohan 6:66-68, "*Kwa ajili ya hayo wengi miongoni mwa wanafunzi wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena. Basi Yesu akawaambia wale thenashara, Je! Ninyi nanyi mwataka*

kuondoka? Basi Simoni Petro akamjibu Bwana! twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele."

Mfano: Ni wale tu walio katika safina wakati wa gharika iliyofunika dunia waliokolewa.

1 Pet. 3:18-20, "*Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa ajili ya hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri; watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji.*"

Neno la Mungu linafundisha hili kuhusu ndani na nje ya Kristo.

- Rum. 8:1, "*Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.*"
- Gal. 3:26, "*Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.*"
- 1 Kor. 15:22, "*Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.*"
- 2 Kor. 5:17, "*Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.*"
- Efe. 1:3, "*Atukuzwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu war oho ndaani yake Kristo;*"

Kulikuwa na mlango mmoja tu katika safina.

- Mwa. 6:16, "*Uifanyie safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, na tatu.*"
- Mwa. 7:16, "*Na walioingia waliingia mume na mke, wa kila kitu chenye mwili, kama vile alivyowamuru Mungu; BWANA akamfungia.*"

Kuna njia moja tu kuingia katika Kristo – kuitii injili.

- 1 Pet. 3:18-21, "*Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri; watu wasiotii hapo zamani uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni ubatizo unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Krsito.*"
- Yohana 10:7-10, "*Bassi Yesu aliwaambia tena, Amin, amin, nawaambieni mimi ndimi mlango wa kondoo. Wote walionitangulia ni wevi na wanyaang'anyi; lakini kondoo hawakuwasikia. Mimi ndimi mlango mtu akiingia kwa mimi, ataokoka; ataingia na*

kutoka, naye atapata malisho. Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuhaaribu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele."

- Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Nataka nikutwe naenenda katika kweli

Kwa mwanamke mteule. 2 Yohana 1:4, "*Nalifurahi mno kwa kuwa nimewaona baadhi ya watoto wako wanaenenda katika kweli, kama vile tulivyopokea amri kwa Baba.*"

Hakusema KUJUA kweli, bali amesema KUENENDA katika kweli.

Ni muhimu kufahamu kweli, lakini pia tunapaswa kueneda katika kweli. Yohana 8:32, "*Tena mtaifahamu kweli, nayo kweli itawaweka huru.*"

Kweli ni nini? Yesu na neno.

- Yohana 14:6, "*Yesu akamwambia, mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"
- Yohana 17:17, "*Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.*"

Nataka nisikutwe nalala

Hii haiongelei usingizi wa kimwili, bali kiroho – kutojielewa, kutofanya kazi, nk.

1 Thes. 5:6, "*Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi.*"

Yesu alifundisha kwamba muda wa kuja kwake ulikuwa haujulikani (Yesu au malaika hawakujua).

Lazima tuwe macho na kukesha. Marko 13:32, "*Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba.*"

Je unahisi kwamba uko macho kwa ajili ya Bwana?

Je unawajibika katika wajibu wako?

Je unatangaza neno la Mungu katika ulimwengu? Marko 16:15, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe.*"

Nataka nikutwe nikiwa macho

"Kuwa macho" ni neno la ufunguo katika huduma ya Yesu.

Maandiko yanalinganisha "kuja kwa mara ya pili" kwa Nuhu na gharika.

Mat. 24:36-44, "*Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake. Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu,*

ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya gharika watu walivyokuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa, , hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wassitambue hata gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Wakati ule watu wawili watakuwako kondeni; mmoja atwaliwa mmoja aachwa; wanawake wawili watakuwa wakisaga; mmoja atwwaliwa; mmoja aachwa. Kesheni basi, kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. Lakini fahamuni neno hili; kama mwenye nyumba angaliijua ile zamu mwivi atakaayokuja, angalikesha wala asingaliiacha nyumba yake kuvunjwa. Kwa ssababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja."

Yesu anatuagiza kukesha na kuomba.

Marko 13:32-33, "*Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba. <u>Angalieni, kesheni</u> [ombeni], kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo.*"

Nataka nikutwe nikiwa tayari

Yesu anaandaa mahali kwa ajili ya waaminifu.

Yohana 14:1-3, "*Msifadhaike mioyoni mwenu mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi kama sivyo ningaliwambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi nanyi mwepo.*"

Ni waliojiandaa tu ndio wataipokea.

Mfano wa wanawali kumi unaeleza hili. Mat. 25:1-13, "*Ndipo ufalme wa mbinguni utakapofanana na wanawali kumi, waliotwaa taa zao wakatoka kwenda kumlaki bwana harusi. Watano wao walikuwa wapumbavu, na watano wenye busara. Wale wapumbavu walizitwaa taa zao, wasitwae na mafuta pamoja nao; basi wale wenye busara walitwaa mafuta katika vyombo vyao pamoja na taa zao. Hata bwana arusi alipokawia, wote wakasinzia wakalala usingizi. Lakini usiku wa manane pakawa na kelele, haya bwana arusi tokeni mwende kumlaki. Mara wakaondoka wanawali wale wote, wakazitengeneza taa zao. Wale wapumbavu wakawaambia wenye busara, tupeni mafuta yenu kidogo; maana taa zetu zinazimika. Lakini wale wenye busara wakawajibu wakisema, sivyo; hayatutoshi sisi na ninyi; afadhali shikeni njia mwende kwa wauzao, mkajinunulie. Na hao walipokuwa wakienda kununua, bwana arusi akaja, nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa. Halafu wakaja na wale wanawali wengine, wakasema Bwana, Bwana tufungulie. Akajibu akasema amini nawaambia siwajui ninyi. Basi kesheni kwa sababu hamwijui siku wala saa.*"

Wengi sana watakutwa wakiwa hawajajiandaa vizuri.

Ni nini kinachomtokea mwanafunzi shuleni akipewa jaribio ambalo hajalisomea? Hawezi kufaulu.

Mkristo anajiandaaje kwa ajili ya kuja kwake Kristo kwa mara ya pili?

Tafuta ufalme kwanza. Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Weka hazina mbinguni. Mat. 6:19-21, "*Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.*"

Nataka nikutwe katika kitabu cha uzima

Ni wale tu walioko katika Kitabu cha uzima ndio watakao okolewa.

Ufu. 20:12-15, "*Nikawaona wafu wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Basi ikawatokea wafu waliokuwamo ndani yake; na mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani hilo ziwa la moto. Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.*"

Jina la mtu linapatikanaje katika Kitabu cha uzima?

Kwa kuzidishwa na Bwana wanapotii injili.

- Mdo. 2:38-40, "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi.*"
- Mdo. 2:47, "*Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Ni muhimu kukutwa ukiwa Mkristo mwaminifu.

Hitimisho

Uko upande gani sasa? Je SASA uko ambavyo unataka Yesu akukute? Huu ndio wakati wa kuwa sahihi na Mungu. Huu ndio wakati wa kufanyika Mkristo.

2 Kor. 6:2, "*(Kwa maana asema, wakati ulikubalika nalikusikia, siku ya wokvu nalikusaidia; tazama wakati ulikubalika ndiyo sasa; tazama siku ya wokovu ndiyo sasa.)*"

Mtu anafanyikaje Mkristo? Mtu ni lazima afanyike Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

. Imani. Waeb. 11:6, "Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu, umri sawa na wa kwangu alikuwa haamini kuwa Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye ana kwa ana kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ili kuwa ni nzuri. Lakini ili kuwa upande ambao ni salama, labda anaweza kwenda kanisani, na kama akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri na kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "mambo haya hayafanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umwamini yeye kwa moyo wako wote, la sivyo huwezi kumpendeza."

. Toba. Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Matend. 11:18, "..... *Mungu amewapa pia mataifa toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa una lala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani humu!" unachukuwa simu na taratibu unawapigia polisi, ukiwambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadilisha maisha yake ili kwamba asiibe tena. Ni badiliko la akili linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya kabla hatujawa Wakristo.

. Kukiri. Warumi 10:9-10*, "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hatakupata haki, na kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu."*

Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Kumbuka kwamba katika somo hilo hapo juu imani (kuamini), toba na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu tayari ameshapata.

. Ubatizo. Ni katika ubatizo ndipo haki inapatikana, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote,

"*Lakini Yohana alitakakumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa alipanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa mpendwa wangu ninayependezwa naye*." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi ya kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni makabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, ulisema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *"Kwa ajili ya ondoleo la dhambi."* Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. *"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni agizo lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Hivyo mnazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale ni lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* (Rum. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatuendi makaburini na kuchukua udongo kidogo na kuweka juu ya mwili wa marehemu.

Kama hujafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo, kwa nini usizingatie leo?